

Mwanamke ni kama hoteli kubwa sana yenye aina nyingi sana za huduma uzipendazo lakini kila chumba kwenye hoteli hiyo kina funguo zake.

Funguo ni kitu kinachokusaidia kufungua mlango ili kupata kuona na kushiriki vitu vilivyopo upande wa pili.

Hivyo kwa kadri unavyozifahamu funguo za vyumba ndivyo unavyoweza kupata **aces** huduma nyingi za hapo hotelini.

Sasa changamoto ya wanaume wengi ni kwamba wanakuwa na funguo moja au mbili na wanalalamika hawahudumiwi vizuri.

Ukitaka kuishi na mwanamke kwa faida na uone raha ya mahusiano yako ukiwa naye ni muhimu

ufahamu ni kwa namna gani unaweza kumfanyia alafu na yeye akafanya vile unavyotaka.

Kwa sababu ni watu wa hisia hivyo wanahitaji kuhamasishwa kwa namna fulani.

Mwanamke anajifunza kwako namna ya kuishi na wewe, vile utakavyomuonyesha upo ndivyo atakavyokuchukulia.

Karibu ujifunze name katika kitabu hiki namna ya kuishi na mwanamke wako.